MZUNGUKO WA PESA

MAELEZO SAHIHI

TAFSIRI ZA KUSAIDIA KUELEWA MZUNGUKO WA PESA KATIKA JUMUIYA YAKO:

- Uchumi: mzunguko wa pesa katika jumuiya yako unategemea uchumi. Uchumi ni njia ambayo bidhaa na huduma huzalishwa na kutumiwa, na rasilimali kusimamiwa katika jamii (uchumi wa mitaani), nchi (uchumi wa taifa), kanda kama Afrika Mashariki (uchumi wa kikanda), au dunia (uchumi wa kimataifa).
- Uchumi wa mitaa, wa kitaifa, wa kikanda na wa kimataifa wote umeunganishwa, na kinachotokea katika eneo moja la uchumi kinaweza kuathiri wengine wote. Kwa mfano, ikiwa kampuni ya kimataifa ya maduka makubwa inafungua tawi katika mtaa, uchumi wa ndani unaweza kuathirika ikiwa watu watatumia pesa zao kidogo kununua bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi na kuuzwa katika maduka madogo-madogo na masoko. Au, kwa mfano, kuongezeka zaidi kwa uzalishaji wa korosho katika nchi ya kigeni kunaweza kuathiri bei na uhitaji wa korosho zinazozalishwa nchini
- Pesa ni rasilimali muhimu katika jamii, na mzunguko wa pesa una athari kubwa katika ustawi wa jamii. Watu wengine wanaweza kufaidika zaidi kuliko wengine kutokana na njia ambazo pesa huzunguka katika uchumi wa ndani.
- Kuna pande mbili za uchumi: uchumi rasmi na uchumi usio rasmi:
  - Uchumi rasmi unamaanisha biashara zote na kazi zinazoendeshwa na taratibu za serikali. Kwa mfano, kampuni za biashara zilizosajiliwa kisheria ni sehemu ya uchumi rasmi. Kazi nyingi zinatolewa na kampuni hizi rasmi, na ajira zao zinaweza kuja na ulinzi wa kisheria na faida kama vile pensheni, likizo wakati wa ugonjwa, na bima ya afya (DESA Working Paper, 2007).
  - Uchumi usio rasmi ni njia zote ambazo watu huzalisha bidhaa na huduma, na kupata pesa, nje ya mazingira rasmi, yanayotakiwa. Wafanyakazi katika uchumi usio rasmi hujumuisha wamiliki wa biashara ndogo-ndogo, wajasiriamali, wafanyakazi wa kujiajiri, wauzaji katika masoko, wafanya vibarua nyumbani au kwenye mashamba na watu ambao hufanya kazi zisizolipwa, kama vile kupika, kusafisha na kulea watoto nyumbani. Programu za maarifa na mafunzo mara nyingi hulenga kuwasaidia vijana kupata kazi rasmi. Sekta isiyo rasmi kiuhalisia inatoa urahisi wa upatikanaji na idadi kubwa ya fursa zaidi za kushiriki katika uchumi wa ndani (Invisible Lives).
- Uchumi rasmi na usio rasmi unaweza kuonekana kuwa tofauti, lakini hutegemeana sana (DESA Working Paper, 2007). Kwa mfano, biashara rasmi ya ujenzi au kiwanda inaweza kuajiri wafanyakazi wasio rasmi na kushirikisha biashara ndogo ili kutoa kazi au huduma fulani inayohitajika. Wakati huo huo kazi za nyumbani zisizolipwa, nguvu kazi katika malezi na kilimo, ambazo mara nyingi hufanywa na wanawake, huwezesha wanajamii wengine kuwa na fursa ya kutoka nje kutafuta ajira zingine zilizolipwa.
- Mnyororo wa thamani ni mfululizo wa hatua ambazo bidhaa, zao au huduma huanza kutengenezwa kwa wazo tu kutoka mwanzo hadi kuwa bidhaa kamili ambayo inaweza kuuzwa kwa wateja katika masoko. Mnyororo wa thamani una hatua nne za msingi: 1) Kubuni bidhaa, 2) Uzalishaji, 3) Kuitangaza kibiashara na 4) Matumizi, Uozeshaji (disposal) na kutumia tena masalia (Recycling) - (Chanzo: Value Chain Handbook). Kwa mfano, mnyororo wa thamani wa mahindi unahusisha 1) Kupata ardhi, mbegu na pembejeo za uzalishaji; 2) Kupanda, kukuza na kuvuna mahindi; 3) Kuuza na kusafirisha mahindi; na 4) kutumika kwa mahindi. Lakini minyororo ya thamani inaweza kuwa ngumu zaidi, hasa ikiwa inahusisha mzunguko tofauti wa uzalishaji. Kwa mfano, mnyororo wa thamani kwa ajili ya uzalishaji wa samani za mbao hushirikisha shughuli tofauti-tofauti kama vile za misitu, upasuaji wa mbao, ujenzi, viwanda, na masoko (ya jumla na rejareja), na pia shughuli za usafirishaji wa bidhaa ili zifikie masoko ya ng'ambo (Chanzo: Value Chain Handbook).
- Kila hatua ya mnyororo wa thamani hutoa fursa tofauti za ajira. Na mnyororo mmoja wa thamani unaweza kuchangia katika kutengeneza minyororo mingine ya thamani. Kwa mfano, mahindi hununuliwa na mteja, kisha kugeuzwa kwa unga ambao unaweza kutumika kutengeneza bidhaa kama vile mkate. Hii inazalisha minyororo mipya ya thamani.
- ' Mjasiriamali wa kilimo ' ni mjasiriamali ambaye

- hujenga thamani kupitia kutengeneza fursa mpya za biashara katika mnyororo wa thamani wa kilimo (Chanzo: Invisible Lives).
- Thamani ya pesa huamuliwa na mahitaji yake, kama vile ilivyo tu na thamani ya bidhaa au huduma. Thamani ya pesa hukuathiri kila siku katika soko. Wazalishaji wanajua unapaswa kununua chakula kila wiki. Si mara zote utaweza kuchelewesha manunuzi yako wakati bei inapoongezeka. Wazalishaji huongeza gharama wanazoingia kwa njia hii.
- Mfumuko wa bei ni wakati thamani ya pesa inazidi kupungua kwa muda. Mara watu wanapotarajia kwamba bei zitaongezeka zaidi, hununua haraka kabla bei hazijapanda. Hali hii huongeza mahitaji, na kuwaarifu wazalishaji kuongeza gharama zao za ziada.
- Kushuka kwa bei (deflation) ni wakati thamani ya pesa inapoongezeka, kumaanisha kwamba bei au gharama ya bidhaa na huduma inashuka. Hii inaweza kuonekana kama ni jambo nzuri, lakini kwa kweli inaweza kuwa na athari kwa kila mtu pia kwa sababu inamaanisha kwamba ardhi, mifugo na mali nyingine hupoteza thamani yao. Ikiwa kila mtu atalipa pesa kidogo tu kwa ajili ya chakula, mavazi na makao yao, inamaanisha kutakuwa kuna pesa kidogo zaidi za kuzunguka katika uchumi wa ndani kuwekeza katika biashara, kutengeneza ajira na kulipa watu mishahara.
- Utumaji pesa (Remittance) ni uhamisho/utumaji wa pesa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, ikiwa mwanafamilia amepata kazi mjini, anaweza kutuma pesa kutoka katika mapato yake ili kusaidia familia yao kijijini. Katika maeneo yenye fursa chache za ajira, utumaji pesa kutoka nje ya jumuiya husika (toka mjini kwenda kijijini kwa mfano) unaweza kuchangia mzunguko wa pesa.

JE, WAJUA?

UCHUMI USIO RASMI NCHINI TANZANIA UNACHANGIA 34% YA UCHUMI WA TAIFA KWA UJUMLA.

67% YA WAFANYAKAZI NCHINI TANZANIA WAMEAJIRIWA KATIKA SEKTA YA KILIMO.

Utafiti katika mji mdogo huko Uingereza uligundua kwamba kila mkaazi angelitumia 1% zaidi ya fedha zao katika uchumi wa ndani, kwa bidhaa na huduma za ndani, basi ingeweza kuingiza £ 52,000,000 ya kutumia mwaka katika uchumi wa mitaa.

(Plugging the Leaks)

NCHINI TANZANIA, WANAWAKE HUCHANGIA 80% YA KAZI ZISIZO NA MALIPO KWENYE MASHAMBA YA FAMILIA.

KUNA TAKRIBAN 17,000 YA WAENDESHAJI WA BIASHARA ZA PESA KWA NJIA YA SIMU WALIOENEA NCHINI TANZANIA, WALIO KATIKA MADUKA, MATAWI YA BENKI, OFISI ZA POSTA NA VITUO VYA MAGARI YA USAFIRI.

JE, WAJUA?

INAAMINIWA KUWA WATANZANIA ZAIDI YA MILIONI 4 WANASHIRIKI KATIKA VIKUNDI TOFAUTI VYA KUWEKA AKIBA, NA KUZALISHA ZAIDI YA BILION 400 ZA TANZANIA KILA MWAKA.

(CARE)

Kuongezeka na kuenea kwa vikundi vya kuweka akiba nchini Tanzania kumepunguza asilimia ya vijana wasioshirikishwa kifedha kutoka 48% hadi 33% katika kipindi cha mwaka 2013 na 2017.

ZAIDI YA WATANZANIA MILIONI 17 BADO HAWAJASHIRIKISHWA KIFEDHA. WENGI WAO NI MABINTI WANAOISHI VIJIJINI.



(CARE)

USHIRIKISHAJI WA KIFEDHA BADO HAUJAWAFIKIA KIKAMILIFU MAKUNDI MADOGO YALIYO KATIKA HATARI. BADO KUNA MAKUNDI YA KAYA NDOGO-NDOGO NCHINI TANZANIA AMBAYO YANAPAMBANA KILA SIKU, WANATEGEMEA MAPATO YAO MADOGO YA KILIMO KWA MAHITAJI YAO, NA KUKOSA ZANA ZA HUDUMA ZA KIFEDHA, HATA ZISIZO RASMI; ILI HALI WANGEPATA FAIDA KUBWA IWAPO MIFUMO YA MSINGI YA KIFEDHA INGEWAFIKIA.

(J. Anderson, C. Marita & D Musiime ; May 2016)]

MIZUNGUKO RASMI NA ISIO RASMI YA PESA

- Fedha inazunguka kwa njia tofauti tofauti katika uchumi rasmi na usio rasmi. Uchumi rasmi huwa na biashara kubwa, ambazo mara nyingi huwa na mitandao midogo na hafifu katika mitaa na uchumi wa mitaani. Kampuni ndogo kwa kawaida huwa zina uhusiano mwema zaidi. (Plugging the Leaks).
- Wanawake wa Tanzania bado wanakabiliwa na ubaguzi kutoka kwa waajiri rasmi. Wanawake wengi zaidi hukosa nafasi za ajira kuliko wanaume, na pia wanawake mara nyingi huajiriwa katika kazi zenye mshahara mdogo au zisizo na malipo katika uchumi usio rasmi.
- Fursa za wanawake na wanaume katika sekta isiyo rasmi huwa na uwezekano tofauti wa mapato kati yao. Fursa zenye mapato makubwa kama vile umiliki mdogo wa biashara mara nyingi huwapendelea wanaume, wakati kazi zile nyingi za nyumbani na za kilimo zisizolipwa zinafanywa na wanawake (Rethinking the Informal Economy, TZ Ministry).
- Kuongezeka kwa huduma za fedha kupitia kwa simu kunaathiri jinsi pesa zinavyozunguka katika jumuiya za Tanzania. Pesa za simu zimeongeza ushirikishaji wa kifedha na kupanua ufikiaji wa huduma za kifedha kwa sekta isiyo rasmi, lakini nyingi ya shughuli hizo za pesa za simu huwa ni kwa ajili ya utoaji wa pesa kati ya wanajamii. (Intermedia).

TAZAMA UCHUMI WA NDANI KAMA NDOO

- Mfano wa ndoo iliyovuja ni njia moja ya kutafakari juu ya jinsi fedha inavyozunguka katika jamii yako. Uchumi wako wa ndani (katika jumuiya) ungekuwa ni ndoo, ni kiasi gani cha pesa ambacho kingeingia ndani ya ndoo hiyo kupitia utoaji wa pesa na mapato ya watu?
- Lengo la mfano wa ndoo iliyovuja inatusaidia kuelewa kinachotokea pesa zinapozunguka katika jumuiya yako - iwe pesa hizo hukaa na kuzunguka katika jumuiya, kadiri watu tofauti wanavyozidi kununua bidhaa na kupata huduma, au aiza huvuja nje ya ndoo na kutiririka mahali pengine.
- Hebu tuangalie mifano miwili ya jinsi matumizi ya watu yanavyoweza kuathiri uchumi wa ndani au wa nje:

  - Fahima huuza kilo 20 za kahawa na kupata TSH 240,000. Kutoka kwenye mapato hayo anatumia TSH 10,000 kwa usafiri (daladala) kufika kwenye duka jipya nje ya mji, ambapo anatumia TSH 50,000 kununua mafuta na mchele vitokavyo ng'ambo, Thailand. Anatoa TSH 100,000 kwa kikundi chake cha akiba ili kuweka ada ya shule ya bintiye; Anatumia TSH 20,000 kununua mboga kwenye soko la mtaani; na ana TSH 60,000 ambazo zimesalia za kuwekeza katika kuandaa shamba la jamii yake kwa ukulima msimu ujao. Ni kiasi gani cha matumizi ya Fahima kinakaa katika uchumi wa ndani, na ni kiasi gani kinachokwenda nje ya nchi (Ng'ambo)?
  - Laetitia ana biashara ndogo ya kuuza maandazi kwenye soko la mtaani. Amepoteza biashara tangu duka kubwa (mall) linalouza vyakula vya kupikwa kwa haraka lilipofunguliwa, lakini anaweza kuongezea mapato yake ya TSH 180,000 kwa TSH 60,000 zaidi kupitia kwa kazi ya kawaida katika duka dogo lililopo mtaani. Kati ya TSH 240,000 aliyo nayo, anatumia TSH 100,000 kununua chakula na bidhaa muhimu kutoka kwa wauzaji wengine; anatumia zingine TSH 30,000 kulipia kusagwa ngano kuwa unga ili apike maandazi yake; yeye humtumia dada yake aliye mjane TSH 100,000 akitumia akaunti yake ya pesa za simu; na anaokoa TSH 30,000 zinazosalia. Je, ni kiasi gani cha matumizi ya pesa za Laetitia hukaa katika uchumi wa ndani (jumuiya) na ni kiasi gani huvuja (hutoka nje ya uchumi wa ndani)?

KUSAIDIA UCHUMI WA NDANI: NDOO KAMILI NA NDOO ILIYOVUJA

- Kupiti mifano hii, tunaweza kuona jinsi kutunza pesa katika jumuiya, kwa mfano kwa njia ya kununua chakula kwenye soko badala ya maduka makubwa makubwa, inaweza kusaidia uchumi wa ndani. Bidhaa zitokazo ng'ambo, au bidhaa zinazouzwa kwenye maduka makubwa ya kimataifa, zinaweza kuwa zina bei nafuu, lakini huumiza kila mtu mwishowe.
- Hebu tutazame mifano miwili tofauti ili tuelewe zaidi:
  - Ndoo kamili: Mwokaji hununua gunia mbili za unga kutoka kwenye mashine ya unga (kinu) ya mtaani. Kwa pesa anazopata kutokana na kuuza unga, mmiliki wa kinu anunua mboga sokoni. Mwanamke anayemuuzia mboga hutumia pesa hizo kununua mandazi kutoka kwa mwanamke mwingine ambaye hupika sokoni. Kwa kupata pesa hizo, mwanamke ambaye hupika maandazi sasa anaweza kushonewa nguo mpya aliyoitamani kwa kutumia mshonaji wa mtaani. Mshoni naye anaweka mapato yake kutoka kweye kushona mavazi ili alipe ada ya shule ya bintiye. Katika mfano huu, mzunguko wa pesa ndani ya jumuiya umeongeza thamani kwa maisha ya kila mtu.
  - Ndoo iliyovuja: Mwokaji alienda dukani kununua unga, na akagundua ya kwamba kuna aina mpya ya unga inayotoka ng'ambo ambayo itamgharimu tu nusu ya kiasi cha pesa ambazo huwa ananunua kutoka kwa kinu mtaani. Akaamua kununua ule unga utokao nje ili kuokoa pesa. Mmiliki wa duka naye akaamua kutumia pesa kutoka kwa uuzaji wa unga kutembelea duka kubwa jipya, na kununua simu. Anapaswa kuamua kama atatumia akiba yake kununua simu au nguo mpya. Simu anayoitaka iko katika ofa maalum mwezi huu, na sasa anaweza kuimudu. Mshoni wa nguo naye anahangaika kupata kazi, kwa hiyo anapanga kuokoa pesa kwa kununua kitambaa kipya cha bei nafuu kitokacho kwenye kiwanda cha ng'ambo. Katika mfano huu, ingawa kila mtu aliokoa pesa katika ununuzi wake, pesa zote ambazo zimetumika zimeondoka kwenye jumuiya, na kuchangia umaskini katika jumuiya hiyo.

PATA UKWELI! ONDOA UPOTOSHAJI!

UPOTOSHAJI	UKWELI
Maduka makubwa ni ishara ya maendeleo na mara nyingi hutoa thamani bora kwa bei nafuu.	Maduka makubwa yanaweza kuuza bidhaa kwa bei nafuu kuliko biashara ndogo mitaani, lakini pesa zile watu wanazotumia kwenye biashara hizo kubwa huenda zikaondoka katika uchumi wa ndani ya jumuiya, na mwishowe kuchangia kwa umaskini wa kila mtu kwenye jumuiya.
Uchumi usio rasmi ni soko haramu na hauchangii maendeleo.	Watu wengi wanahusika katika uchumi wa ndani kupitia kwenye njia ya uchumi usio rasmi. Unawezesha ujasiriamali na uundaji wa biashara ndogo-ndogo katika kila hatua ya mnyororo wa thamani. Kazi nyingi zisizolipwa hufanyika katika uchumi usio rasmi, kama vile malezi ya watoto, ambayo inachangia kwa ustawi wa jamii na jumuiya.
Kilimo sio biashara endelevu	Kilimo ni mojawapo ya sekta nzuri kwa vijana kushiriki katika uchumi wa ndani, na inatoa fursa nyingi mpya za ujasiriamali katika mnyonyoro wa thamani (Invisible Lives)
Wanaume wanafanya kazi zaidi katika kilimo kuliko wanawake	Ukweli: 52% ya wafanyakazi katika sekta ya kilimo nchini Tanzania ni wanawake.

KUUNGANISHA NGUVU ZA VIKUNDI VYA AKIBA NA HUDUMA ZA PESA KWA SIMU YA MKONONI

- Tanzania ina moja ya huduma bora ya ubunifu na ushindani katika masoko ya huduma za pesa kwa njia ya simu duniani.
- Tanzania ina utamaduni hai na unaoendelea kukua wa vikundi visivyo rasmi vya kuweka akiba ambapo kuna zaidi ya wanachama milioni 4.
- Makundi yote ya huduma za pesa kwa njia ya simu pamoja na vikundi vya akiba yanaweza kuokoa hali ya umaskini katika jumuiya za vijijini ambazo ziko nyuma katika kupatiwa vizuri huduma na bidhaa na taasisi za kifedha. Pesa zilizotumwa kupitia simu za mkononi na miundo inayotolewa na makundi ya akiba hu-wawezesha watu kusimamia mahitaji yao kwa misimu tofauti, kama vile kulipa ada za shule kwa wakati fulani wa mwaka, kuishi katika vipindi vya mavuno pungufu, na kwa mambo yasiyotarajiwa kama mtu kuwa mgonjwa katika familia.

NYENZO YA RASILIMALI ENDELEZA UTAFITI WAKO!

- **https://www.ted.com/talks/niti_bhan_the_hidden_opportunities_of_the_informal_economy**
- **https://www.ted.com/talks/ngozi_okonjo_iweala_how_africa_can_keep_rising**
- **http://www.uncdf.org/article/2700/rfa-enhancing-livelihoods-through-savings-groups-in-tanzania**
- **http://www.mcdgc.go.tz/index.php/publications/more/gender_and_economic_growth_in_tanzania_creating_opportunities_for_women/**

MZUNGUKO WA PESA

MWONGOZO WA UZALISHAJI WA VIPINDI VYA REDIO

MWONGOZO WA KUTAYARISHA KIPINDI CHA REDIO
MZUNGUKO WA PESA

MAANDALIZI YA KIPINDI

NJIA TOFAUTI ZA KUZUNGUMZIA MZUNGUKO WA PESA / THAMANI/MISINGI YA PESA KATIKA JUMUIYA YAKO

- Kuelewa jinsi pesa kwa njia ya simu za mkononi (mobile money) inaathiri mtiririko na mzunguko wa pesa katika jumuiya yangu
- Minyororo ya thamani muhimu katika jamii yangu: ni jinsi gani inafanya kazi na kuchangia katika uchumi wa ndani (ya jumuiya)
- Ndoo iliyovuja: kuelewa mtiririko na mzunguko wa fedha na kuunda thamani katika jamii yangu
- Uhusiano kati ya uchumi rasmi na isiyo rasmi katika jamii yangu

CHAGUA MADA MAHUSUSI

Mzunguko wa fedha na kuunda thamani/msingi katika jamii yako: maswali ya kuzingatia

- Vyanzo vya pesa katika jumuiya yako ni vipi?
- Je, ni kiasi gani cha pesa zako kinakaa katika uchumi wa ndani (Jumuiya/mtaani)?
- Je, biashara katika mitaa zina nguvu sana katika jumuiya yako? Ni nini kinachowawezesha kustawi na kukua? Wanakabiliwa na vitisho? Wanaongezea thamani gani kwa jumuiya?
- Je, ni uhusiano na viunganishi (links) vipi vinavyowezesha pesa kubakia na kuendelea kuzunguka katika jumuiya yako?
- Ni watu gani wanaofanya kazi katika uchumi usio rasmi / rasmi -- Je, hii ni kweli? Ni maoni gani potofu?
- Je, kuna uhusiano wa kijinsia katika mzunguko rasmi na usio rasmi wa pesa?
- Wewe hununua nini? Imetoka wapi? Imetengenezwa wapi na ni nani?
- Ni nini chaguo lako au mambo unayozingatia linapokuja suala la kununua vitu?
- Ni bidhaa gani zinazozalishwa katika jumuiya yako? Shughuli hizi huungwaje mkono?
- Je, ni changamoto na fursa zipi za kutengeneza utajiri / thamani katika jumuiya yako? Kuna vikwazo vya umri au jinsia?
- Nani hufanya kazi isiyolipwa katika jumuiya yako? Je, michango yao hutambuliwa au la? Ni thamani gani inatengenezwa kupitia shughuli hizi?

MIUNDO YA REDIO

SAUTI YA UMMA

Lengo la sauti ya umma
Kupata maoni mengi juu ya mada moja.

Utazungumza na nani?
Mtu yeyote kutoka kwa jamii

Swali
Je, wewe hununua nini iliyotengenezwa (au kukuzwa) nchini?

MAONI YA SAUTI

Maoni ya sauti yanalenga
Kupata maoni ya watu juu ya mada ambayo wanayoijali sana.

Utazungumza na nani
Mkulima au mfanyibiashara wa eneo hilo ambaye anashindana na bidhaa za bei nafuu zinazoletwa nchini kutoka ng'ambo.

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa sauti
Kupata simulizi ya mtu aliye na uzoefu au shauku katika jambo fulani. Mara nyingi muundo wasifu wa sauti unatumika kwa kuhamasisha wengine.

Utazungumza na nani
'Mmiliki wa kilimo' au mmiliki wa biashara katika jumuiya aliyechagua kuwekeza katika uchumi wa ndani kwa kutengenezea bidhaa ndani ya nchi. Waulize wazungumzie juu ya changamoto wanazokabiliana nazo, mahusiano au mifumo ya usaidizi inayowawezesha kukaa katika biashara, malengo yao na maono kwa jamii.

Maswali ya kuuliza kabla ya kuanza kurekodi ili kumsaidia mhusika kufikiria wasifu au simulizi yake

- Ni nini kilichokufanya ukataka kuendeleza biashara ya ndani?
- Je, unashiriki katika mnyororo gani wa thamani?
- Umekumbana na changamoto gani?
- Unaonaje nafasi yako katika jamii na uchumi wa jumuiya?
- Je, unafikiri ni thamani gani imetengenezwa/imezalishwa kupitia katika biashara yako?
- Je, wewe unashindanaje na biashara kubwa?
- Kwa nini ni muhimu watu kuunga mkono biashara yako ikiwa bidhaa kama hizo zinaweza kupatikana kwa bei nafuu mahali pengine?
- Je, mawazo yako yamebadilika kuhusu maana ya kushiriki katika uchumi wa ndani ya jumuiya?
- Je, ni jambo gani muhimu zaidi ulilojifunza kuhusu ujenzi wa biashara ya ndani iliyostawi?

TAFADHALI ANGALIA MASWALI YA MAHOJIANO KATIKA SEHEMU YA "JINSI YA KUANDAA KIPINDI"

TANGAZO LA UMMA

Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

VIDOKEZO VYA UWASILISHAJI

Unda Tangazo la Umma linalowahimiza watu kuunga mkono biashara ya ndani au kuinua ufahamu kuhusu "ndoo iliyovuja"

JINSI YA KUENDESHA KIPINDI

Tumia vipengele, utafiti wako, muongozo uliopendekezwa na maswali kuandika muongozo wako mwenyewe.

[KUFUNGUA KIPINDI:]
Mtangazaji 1: Imetimia saa [MUDA] na ni wakati wa [JINA LA KIPINDI] kwenye [JINA LA REDIO]. Jina langu ni [JINA].

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [JINA], na kipindi cha leo ni kuhusu kuelewa thamani ambayo inatengenezwa/inatokana na uchumi wa ndani! Hiyo ni kweli, tutazungumzia jinsi maamuzi yako kuhusu unachokiuza au kununua yanavyochangia, na kama pesa uitumiayo hubaki ndani ya jumuiya yako na inaweza kuwa na matokeo makubwa kwa jumuiya.

Mtangazaji 1: Ni kweli, tutazungumza kuhusu umuhimu wa watu kuelewa athari kubwa ya matumizi yao. Hebu fikiria, kama ningeenda kununua chakula na mavazi yangu yote kutoka kwenye maduka mapya makubwa-makubwa, hakuna jinsi ya pesa nilizozitumia kuweza kurudi kwenye mzunguko wa jumuiya au kwa watu wanaoishi katika jamii yangu. Pesa hizo zitaenda nje kusaidia kampuni kubwa ziwe tajiri, na jumuiya yangu ndio itakuwa imepoteza.

Mtangazaji 2: Leo, tutazingatia uchumi wa ndani kama ndoo iliyovuja, na kuelewa unachoweza kufanya ili kuziba uvujaji wa pesa kutoka kwa jumuiya yako. Tunakuletea taarifa nyingi zinazohitajika ili kuanza mazungumzo kuhusu jinsi ya kuhifadhi matumizi ya pesa katika jumuiya zetu.

Mtangazaji 1: Hebu tusikie zaidi juu ya kile ambacho watu wanafikiria kuhusu kushikilia thamani ambayo imeundwa katika uchumi wa ndani.

[TAMBULISHA MGENI ANAYEHOJIWA]

[CHEZA MAHOJIANO]

[FUNGA KIPENGELE]

Mtangazaji 1: Leo tumejifunza yote kuhusu jinsi tunavyoweza kufaidika na kuungana pamoja ili kujenga uchumi wetu wa ndani ya jumuiya zetu.

Mtangazaji 2: Naam! Tunaweza tukawa tunaishi katika ulimwengu wa utandawazi, lakini sasa tunaona umuhimu wa uchumi wa mitaa ni bora kwa maisha yetu, na nini tunaweza kufanya ili kusaidia kutunza uchumi huu wetu wa ndani.

Mtangazaji 1: Hadi wiki ijayo, siku ya [TAJA SIKU] saa [MUDA]. Tutazungumza kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati huo, kwaheri kutoka kwetu!

MUUNDO AU MPANGILIO WA KIPINDI



MAADILI NA IDHINI/ RIDHAA

Hakikisha umewafahamisha wasikilizaji kuwaheshimu wale wanaotoa hadithi zao binafsi.

MPANGILIO WA SHUGHULI ZA KUFIKIA JAMII

Unapopanga shughuli yako ya kufikia jamii, tahadhari nishati ambayo shughuli
fulani huzalisha ili uepuke kuanza kwa kishindo na kisha kumalizia kwa wepesi.